# Lugha ya mtoto kuanzia miezi 6 hivi

## Machache kuhusu lugha ya mtoto wako kuanzia miezi 6

- Mtoto wako ana mengi ya kugundua ulimwenguni! Tazama kile mtoto anachoangalia na mwambie mtoto jina la kile kitu. Angalia kila kitu kinachosisimua, kidogo na kikubwa, kwa pamoja!
- Hata sasa, mtoto wako anawasiliana na wewe kwa kutumia sura za uso, sauti na mwili. Hivi karibuni, mtoto ataanza kutumia sauti zinazofanana na maneno kama vile da-da na ta-ta.
- Pole kwa pole mtoto anaanza kuelewa misemo kama vile angalia na maneno kama vile mama na baba.
- Mtoto wako anapenda kuongea na wewe, kucheza mchezo wa kuficha uso na kufuatana katika michezo rahisi ya kutumia mwili kama vile Buibui Imse Vimse [Imse vimse spindel] na Oka keki ndogo [Baka baka liten kaka].

## Zungumza kuhusu kila kitu

Zungumza na mtoto wako kuhusu kila kitu kinachotendeka na kinachompendeza mtoto wako. Zungumza kuhusu chakula, nguo, vitu mnavyoona na kile ambacho mtoto anafanya. Msikilize mtoto kwa umakini, na mtoto atapenda kuendelea na mazungumzo. Mpe muda wa kutosha!

## Badilishana na kurudiarudia

Kurudia sauti ya mtoto, kisia maana yake na kusema hayo kwa sauti. Subiri mtoto ajibu kwa sauti au ishara za mwili kabla ya kuendelea. Mtoto tayari anajifunza kuchukua zamu kuzungumza na kuelewa uhusiano kati ya maneno na vitu.

## Fanya lugha kuwa mchezo

Imba nyimbo, mashairi na mashairi yenye vina na cheza michezo ya nyimbo. Tumia vidole vya mikono na vidole vya miguu, toa sauti nyembamba na nene ukichekesha! Kwenye maktaba kuna vitabu, nyimbo na muziki wa kuazima nyumbani.

## Zungumza-soma pamoja

Wakati mtoto anaweza kufuata macho yako na kuangalia kitu unachoashiria kwenye kitabu chenye picha, kitabu kitamfurahisha. Onyesha na kueleza kuhusu picha. Uwe makini ili uone ni nini kinachompendeza mtoto. Mwanzoni, upendezi utakuwa wa muda mfupi, lakini baada ya muda uwezo wa mtoto wa kuwa makini utaongezeka.

## Ongea lugha yako ya asili

Ongea, imba na usome kwa lugha yako ya asili. Watoto wengi ulimwenguni wanaishi katika mazingira ya lugha nyingi, na kuna faida tu za kulelewa na lugha zaidi ya moja.

### Pata maelezo zaidi

- Soma zaidi kuhusu Bokstart hapa: www.bokstart.se
- Ikiwa una wasiwasi kuhusu maendeleo ya lugha ya mtoto wako, wasiliana na Kituo cha afya ya watoto. Unaweza kujadili maendeleo ya lugha ya mtoto wako pamoja na wafanyakazi wa Shule ya mapema.

Baraza la Utamaduni lina jukumu la serikali kuhamasisha usomaji na kuchochea maendeleo ya lugha ya watoto wadogo. Bokstart ni mradi wa kitaifa unaolenga wazazi na watu wazima wanaoshughulika na watoto.

Bokstart

Swahili

# Lugha ya mtoto kuanzia mwaka 1 hivi

## Machache kuhusu lugha ya mtoto wako kuanzia mwaka 1

- Mtoto hutumia ishara na sauti kukuambia jambo fulani.
- Maneno ya kwanza yanahusu hapa na sasa, kama vile mpira, dubu na angalia.
- Mtoto wako anaelewa maneno mengi kuliko anavyoweza kusema lakini anahitaji usaidizi wako ili kuelewa na kusema.

## Fuatilia upendezi wa mtoto

Unaweza kutumia kila kitu unachokiona na kufanya katika maisha ya kila siku ili kuendeleza lugha ya mtoto. Sema jina la kitu ambacho mtoto anaangalia sasa hivi. Wakati mtoto anasema pale, na ananyosha kidole kuonyesha paka, unaweza kujibu: Ndiyo, ni paka. Je, unampenda paka? Kumbuka kusubiri jibu la mtoto.

## Uwe makini na sikiliza

Unapompa mtoto uangalifu wako na kumsikiliza kwa makini, mtoto atahisi kwamba ujumbe wake ni muhimu kwako, iwe mtoto anasema neno, kuonyesha kitu, au kuwasiliana nawe kwa njia nyingine. Unapomjibu mtoto, atajifunza kwamba mnapokezana wakati wa mazungumzo.

## Cheza na lugha

Imba nyimbo, mashairi na mashairi yenye vina na cheza michezo ya nyimbo. Tumia vidole vya mikono na vidole vya miguu, toa sauti nyembamba na nene ukichekesha!

## Tunga hadithi

Eleza kile mwanasesere wa mtoto anachofanya au basi la nje linaenda wapi. Zungumza kuhusu picha za familia na marafiki. Mtoto anahitaji kusikia maneno mapya mara kadhaa, katika mazingira tofauti.

## Soma vitabu rahisi vya picha

Sasa unaweza kuanza kutumia vitabu vya picha. Mwanzoni mtatazama picha pamoja na kumwonyesha vitu kwa kidole. Mara ya kwanza ni rahisi zaidi unaposimulia hadithi mwenyewe, lakini hatimaye mtoto anaweza kusikiliza ukisoma maandishi ya kitabu. Kwenye maktaba kuna vidokezo kuhusu vitabu vya kuazima nyumbani.

## Ongea lugha yako ya asili

Ongea, imba na usome kwa lugha yako ya asili. Watoto wengi ulimwenguni wanaishi katika mazingira ya lugha nyingi, ni faida tu za kulelewa na lugha zaidi ya moja.

## Pata maelezo zaidi

- Soma zaidi kuhusu Bokstart hapa: www.bokstart.se
- Ikiwa una wasiwasi kuhusu maendeleo ya lugha ya mtoto wako, wasiliana na Kituo cha afya ya watoto. Unaweza kujadili maendeleo ya lugha ya mtoto wako pamoja na wafanyakazi wa Shule ya mapema.

Baraza la Utamaduni lina jukumu la serikali kuhamasisha usomaji na kuchochea maendeleo ya lugha ya watoto wadogo. Bokstart ni mradi wa kitaifa unaolenga wazazi na watu wazima wanaoshughulika na watoto.

Bokstart

Swahili

# Lugha ya mtoto kuanzia miezi 18 hivi

## Machache kuhusu lugha ya mtoto wako kuanzia miezi 18 hivi

- Watoto wengi wa umri huu wanaelewa maneno ya kila siku 200 hivi.
- Mtoto hutumia baadhi ya maneno mwenyewe, lakini maneno yanaweza kumaanisha mambo tofauti katika miktadha tofauti.
- Watoto wengine huanza kuunganisha maneno, kwa mfano gari mama au mbwa pale.

## Zungumzeni sana

Ongea kuhusu kile unachofanya katika hali tofauti. Mwambie mtoto kile kinachotendeka na eleza kwa maneno kile unachofanya. Sikiliza kwa makini kile mtoto anachofikiri na maoni yake. Mpe mtoto wako wakati mwingi.

## Hakikisha na kuendeleza kile mtoto anasema

Unapotumia maneno ya mtoto mwenyewe na kuongeza mapya, unamsaidia mtoto kukuza lugha yake. Ikiwa mtoto anasema «namnam», unaweza kusema: Ndiyo, ni chakula na sasa tutakula. Kama mtoto anasema aka badala ya paka ni kawaida kwa umri huu. Usimsahihishe mtoto, lakini tumia neno paka mwenyewe ili mtoto asikie jinsi linapaswa kutamkwa.

## Husisha maneno na mtoto mwenyewe

Ni rahisi zaidi kujifunza mambo mapya ikiwa unaunganisha neno na kitu ambacho mtoto tayari anajua. Ikiwa mnaangalia picha ya suruali, unaweza kuashiria suruali ya mtoto mwenyewe na kusema: Wewe pia una suruali, kama mtoto katika kitabu.

## Zungumza-soma pamoja

Mtoto sasa anafurahia vitabu vingi tofauti ambavyo mnaweza kuvizungumzia pamoja. Uliza maswali wazi kuhusu kile kinachotendeka katika vitabu kulingana na uzoefu wa mtoto: Unafikiri nini...? Unakumbuka…?

## Ongea lugha yako ya asili

Ongea, imba na usome kwa lugha yako ya asili. Watoto wengi ulimwenguni wanaishi katika mazingira ya lugha nyingi, ni faida tu za kulelewa na lugha zaidi ya moja.

## Pata maelezo zaidi

- Soma zaidi kuhusu Bokstart hapa: www.bokstart.se
- Ikiwa una wasiwasi kuhusu maendeleo ya lugha ya mtoto wako, wasiliana na Kituo cha afya ya watoto. Unaweza kujadili maendeleo ya lugha ya mtoto wako pamoja na wafanyakazi wa Shule ya mapema.

Baraza la Utamaduni lina jukumu la serikali kuhamasisha usomaji na kuchochea maendeleo ya lugha ya watoto wadogo. Bokstart ni mradi wa kitaifa unaolenga wazazi na watu wazima wanaoshughulika na watoto.

Bokstart

# Lugha ya mtoto kuanzia miaka 3 hivi

## Machache kuhusu lugha ya mtoto wako kuanzia miaka 3

- Watoto wengi wanaelewa maneno mia kadhaa sasa. Wanaunganisha maneno na kuunda sentensi na kuanza kuzungumza kifupi.
- Mtoto anauliza maswali mengi na anaanza kuelewa jinsi ya kutumia maneno na kucheza nayo.
- Mtoto wako anaanza kukuelezea mambo aliyepitia na anapenda kusikiliza unapoongea.

## Kugundua herufi na maneno

Katika umri wa kwenda Shule ya mapema, watoto wengi wanatamani kujua herufi na maneno. Soma na uashirie kwenye vibao na paketi wakati mtoto anaonyesha kupendezwa. Gundua ishara na alama katika mazingira na kuzungumza kuhusu maana yazo.

## Fafanua maneno mapya

Ni vizuri kutumia maneno mapya kwa kile kinachotendeka na yale mnayoona katika maisha ya kila siku. Fafanua maneno ambayo mtoto haelewi: bahari ni aina ya ziwa, ni kubwa zaidi tu. Au: tunapoenda pwani, tunaogelea baharini.

## Zungumzeni

Zungumzia mambo mliyofanya siku hiyo. Fuatilia jambo ulilosikia au kuona mtoto akifanya kwenye Shule ya mapema na umtie moyo aeleze zaidi.

Watoto wengi wa miaka mitatu hawawezi kutamka maneno yote kama sisi watu wazima. Mtoto akitamka neno fulani vibaya, unaweza kutamka kwa usahihi na hatimaye mtoto atajifunza kutamka vizuri.

## Soma pamoja

Jenga mazoea ya kusoma kidogo kila siku. Watoto wengi wana kitabu wanachokipenda sana ambacho wanataka kisomwe tena na tena. Chagua vitabu vya picha vyenye hadithi ngumu zaidi sasa, lakini bado ni utasoma kwa njia ya mazungumo.

Mtie moyo mtoto kuzungumza kuhusu hadithi ya kitabu na kuliza maswali wakati huo huo. Mtoto anapouliza, tua, sikiliza na kufikiria pamoja.

Kumbuka kwamba kucheza ni njia ya mtoto ya kujifunza. Kwa hiyo cheza, soma, imba na kuzungumza pamoja. Mashairi, mashairi ya vina na nyimbo bado zinafurahisha. Kusoma vitabu ni njia bora ya kujifunza maneno mapya!

## Ongea lugha yako ya asili

Ongea, imba na usome kwa lugha yako ya asili. Watoto wengi ulimwenguni wanaishi katika mazingira ya lugha nyingi, ni faida tu za kulelewa na lugha zaidi ya moja.

### Pata maelezo zaidi

- Soma zaidi kuhusu Bokstart hapa: www.bokstart.se
- Ikiwa una wasiwasi kuhusu maendeleo ya lugha ya mtoto wako, wasiliana na Kituo cha afya ya watoto. Unaweza kujadili maendeleo ya lugha ya mtoto wako pamoja na wafanyakazi wa Shule ya mapema.

Baraza la Utamaduni lina jukumu la serikali kuhamasisha usomaji na kuchochea maendeleo ya lugha ya watoto wadogo. Bokstart ni mradi wa kitaifa unaolenga wazazi na watu wazima wanaoshughulika na watoto.

Swahili

Bokstart